**MUHTASARI WA KIKAO CHA TATU CHA BODI YA ZABUNI KUJADILI TAARIFA YA TATHMIN ZA UJENZI WA EMD NA NYUMBA YA WATUMISHI (THREE IN ONE SEMI DETACHED STAFF HOUSE URBAN TYPE) KATIKA HOSPITALI YA WILAYA YA ITILIMA KILICHOFANYIKA TAREHE 19/01/2022.**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Michael Tolage | DHRO | K/Mwenyekiti |
| 2. | Happiness T. Komba | Ag: HPMU | Katibu |
| 3. | Dkt. Anold Musiba | DMO | Mjumbe |
| 4. | Mateso Kaswanu | DAICO | Mjumbe |
| 5. | Mtobi K. Edward | DEO | Mjumbe |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Amina Mbwambo | DCDO | Kwa taarifa |

**AGENDA**

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha muhtasari wa kikao kilichopita
3. Kujadili taarifa ya tathmin Ujenzi wa EMD na Nyumba ya watumishi (Three in One Semi Detached Staff House Urban Type.
4. Kuahirisha kikao.

**AGENDA: 1/19/01/2022: KUFUNGUA KIKAO**

K/Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni alifungua kikao mnamo saa 04:25 Asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe wote waliohudhuria.

**AGENDA: 2/19/01/2022: KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA**

Wajumbe walisomewa muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 16/12/2021 na waliuthibitisha kuwa muhtasari halali na ulisainiwa.

**AGENDA: 3/19/01/2022: KUJADILI TAARIFA YA TATHMIN UJENZI WA "EMERGENCY MEDICAL DEPARTMENT BUILDING" NA "THREE IN ONE SEMI DETACHED STAFF HOUSE URBAN TYPE".**

Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa amepokea taarifa ya tathmin kutoka kwa kamati ya tathmin inayohusu ujenzi wa "EMD", na ujenzi wa nyumba ya watumishi (Three in one semi detached Staff Urban type) ambapo walioteuliwa kufanya tathmin hizo ni:

1. Eng. Mussa Ezekiel Mwenyekiti
2. Magreth Mabebe Katibu
3. Eng. Frank Tairo Mjumbe.

Scanned with CamScanner

4. Tech. Justine Mwita Mjumbe
5. Tech. Veronica Lwiva Mjumbe,

Kamati ya tathmin walifanya kazi hizo kwa hatua tatu (3)

i. Preliminary Examination
   - Zabuni imesainiwa na anayehusika
   - Power of Attorney
   - Bid securing declaration
   - CRB Registration
   - TIN/VAT Certificate

ii. Detailed Bid Examination and price comparison
   - Hesabu zao kama ziko sawa zilizojazwa kwenye BOQ
   - Ulinganisho wa bei (mwenye bei ndogo kuliko wote)
   - Mpango kazi

iii. Post qualification Evaluation.
   - Uzoefu wa kufanya kazi za ujenzi
   - Mitambo na vifaa vya kufanyia kazi
   - Elimu na uzoefu wa wafanyakazi
   - Uwezo wa kifedha

Baada ya kupitia vigezo vyote hapo juu kamati ya tathmin ilimpendekeza G E Engineering and construction kufanya kazi ya ujenzi wa nyumba ya watumisi kwa gharama ya Tshs 212, 014,100 bila VAT na Yire Ladder Co. Ltd kufanya kazi ya ujenzi wa "Emergency Medical Department Building" kwa gharama ya Tshs 610,883,700.00 bila VAT.

Fedha walizotenda /walizojaza wazabuni zipo juu kuliko fedha tulizopokea .

**Maamuzi ya Wajumbe katika kikao cha Bodi:**

Wajumbe walijadili kwa kina na kuridhia kwamba, itumike njia ya ununuzi ya "force account" kwa vile tumepata kibali cha kutukeleza mradi kutoka TAMISEMI. Kitengo cha manunuzi kihakikishe taratibu zote za force account zinafuatwa kwa kutumia shilingi milioni mia tatu (**Tshs: 300,000,000/=**) kwa ujenzi wa **EMD** na shilingi milioni Tisini (**Tshs: 90,000,000/=**) kwa ujenzi wa nyumba ya watumishi hospitali ya wilaya ya Itilima.

Scanned with CamScanner

**AGENDA: 3/19/01/2022: KUAHIRISHA KIKAO**

Mwenyekiti aliahirisha kikao cha bodi ya zabuni mnamo saa 05:10 Asubuhi kwa kuwashukuru wajumbe wote waliohudhuria.

Saini ..........................................

Tarehe 8/2/2021

Jina Mlobi K. Edward

**Mwenyekiti**

Saini ..........................................

Tarehe 08/02/2022

Jina Happiness T. Komba.

**Katibu**

Scanned with CamScanner

**MUHTASARI WA KIKAO CHA PILI CHA BODI YA ZABUNI KUJADILI ZABUNI ZA UJENZI WA EMD NA NYUMBA YA WATUMISHI (THREE IN ONE SEMI DETACHED STAFF HOUSE URBAN TYPE) KATIKA HOSPITALI YA WILAYA YA ITILIMA KILICHOFANYIKA TAREHE 16/12/2021**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Amina A. Mbwambo | DCDO | Mwenyekiti |
| 2. | Happiness T. Komba | Ag: HPMU | Katibu |
| 3. | Dkt. Anold Musiba | DMO | Mjumbe |
| 4. | Mateso Kaswanu | DAICO | Mjumbe |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mtobi K. Edward | DEO-Sekondari | Kwa taarifa |

**AGENDA**

1. Kufungua kikao
2. Kujadili Ujenzi wa EMD na Nyumba ya watumishi (Three in One Semi Detached Staff House Urban Type.
3. Kuahirisha kikao.

**AGENDA: 1/16/12/2021: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni alifungua kikao mnamo saa 03:40 Asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe wote waliohudhuria.

**AGENDA: 2/16/12/2021: KUJADILI UJENZI WA "EMERGENCY MEDICAL DEPARTMENT BUILDING" NA "THREE IN ONE SEMI DETACHED STAFF HOUSE URBAN TYPE".**

- **UJENZI WA "EMERGENCY MEDICAL DEPARTMENT BUILDING" NA "THREE IN ONE SEMI DETACHED STAFF HOUSE URBAN TYPE".**

Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri imepokea fedha kwa ajili ya ujenzi wa "EMD" na "Three in One Semi Detached Staff House Urban type na kitengo cha Manunuzi kimepokea "BOQ" za kazi tajwa kutoka kwa Mhandisi wa Wilaya na kuzitengenezea Vitabu vya zabuni hivyo basi aliwaomba wajumbe kujadili Zabuni hizo na kuchagua njia ya ununzi itakayotumika kwa kazi hizo na njia hiyo iwe fupi kwa ajili ya kukamilika haraka kwa mchakato wa manunuzi.

Scanned with CamScanner

Kitengo cha Manunuzi kilishauri itumike njia ya "Restricted Tendering" kwa wazabuni wafuatao wa "Class four" (4) kwa kupewa vitabu vya Zabuni.

1. M/S G. E ENGINEERING CO. LTD
2. M/S ROSLAC ENGINEERING CO. LTD
3. M/S YIRE LADDER CO. LTD
4. M/S BEST ONE LTD

**Maamuzi ya Wajumbe katika kikao cha Bodi:**

Wajumbe walijadili kwa kina na kuridhia itumike njia ya "Restricted Tender" kwa wazabuni tajwa hapo juu kupelekewa vitabu vya Zabuni, tarehe ya Kuwaarika iwe 17/12/2021 na kufungua/mwisho wa kupokea tarehe 30/12/2021.

**AGENDA: 3/16/12/2021: KUAHIRISHA KIKAO**

Mwenyekiti aliahirisha kikao cha bodi ya zabuni mnamo saa 05:20 Asubuhi kwa kuwashukuru wajumbe wote waliohudhuria.

Saini ..........................................

Tarehe ....19/01/2022....

Jina ....Michael Tinkaye....

**Mwenyekiti**

Saini ..........................................

Tarehe ....19/01/2022....

Jina....Happiness T. Komba....

**Katibu**

Scanned with CamScanner

16/12/2021

# MAHUDHURIO YA WAJUMBE WA BODI YA ZABUNI

| NA | JINA | CHEO | SAHIHI |
| --- | --- | --- | --- |
| 1 | AMINA MBWAMBO | M/KITI | [signature] |
| 2. | Mateso P. Kaswanu | Mjumbe | [signature] |
| 3 | Denis Kisaye | Secretariat | [signature] |
| 4. | DKT. ANOLD C. MUSIBA | Mjumbe | [signature] |
| 5. | HAPPINESS I. KOMBA | Katibu | [signature] |

Scanned with CamScanner